



Tausi alikuwa ndege mpole.
Aliishi na ndege wenzake vizuri.





Tausi hakuweza kupaa ili auone
uzuri wa dunia kama
ndege wengine.



Hakuweza pia kwenda mbali kutafuta chakula.
Ndege wengine walimcheka. Walimwacha Tausi
kila walipoenda kutafuta chakula.





Tausi alijisemea, “Kama na mimi ni ndege, basi ninaweza kupaa. Ni lazima nipae.”
“Lakini mimi sina mabawa kama wenzangu, nitawezaje kupaa?” Tausi aliwaza.



Tausi alipata mbinu.
Alianza kukusanya
manyoya ya ndege
wengine.



Alianza kwa kumvizia
bundi aliyekuwa
amelala na kumtoa
manyoya.

Alipata manyonya
mazuri, marefu na
meusi.



Alipoenda kwa kasuku
kwa ujanja alimtoa
manyoya machache.

Manyoya ya kasuku
yalikuwa ya rangi ya
kijani na manjano.



Kwa muda mrefu,
ujanja wa tausi
haukujulikana.

Aliutumia pia kupata
manyoya ya bata
bukini. Alimkuta
anaogelea mtoni,
akanyata na kupata
manyoya mazuri
meupe.



Tausi alitumia mbinu hadi akapata manyoya ya tai pia. Alimvizia alipokuwa anakula mzoga.



Alikusanya manyoya
mengi ya rangi
mbalimbali.
Akayaunga na
kutengeneza manyoya
marefu ya rangi
tofauti.



Alijibandika manyoya yale. Alipoutanua mkia wake, ulichanua kama feni.

Ulipendeza na kuvutia kwa rangi mbalimbali alizokuwa nazo.



Tausi alipata manyoya
na mkia uliovutia.
Uzuri wa mkia wake
uliwazidi ndege wote.




Tausi alikuwa na furaha sana. Alipata mkia mzuri na unaovutia. Hakutaka tena kujifunza kupaa. Ndege wengine walivutiwa na uzuri wake.



This book was made possible by Pratham Books' StoryWeaver platform. Content under Creative Commons licenses can be downloaded, translated and can even be used to create new stories - provided you give appropriate credit, and indicate if changes were made. To know more about this, and the full terms of use and attribution, please visit the following [link](#).

Images Attributions:

Disclaimer: https://www.storyweaver.org.in/terms_and_conditions



Some rights reserved. This book is CC-BY-4.0 licensed. You can copy, modify, distribute and perform the work, even for commercial purposes, all without asking permission. For full terms of use and attribution, <http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/>